**Dondoo za Mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam**
**26 Julai 2008**

**Waliohudhuria**

Ally Saidi Mohamedi
Ally Saidi Mwishehe
Amar Shanghavi
Aseli Wilison
Bashiri Rashidi
Dominata Rwechungura
Edgar R Paulo
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Frank Peter Rwechungura
Husein Hamza Hamisi
Juma Imori Rugole
Jumanne Idd Selemani
Kibwana Mohammad Msiga
Mussa Alex
Mussa Omari
Nickson Kilunga
Paulo Atibu Hatibu
Solomon Mihoyo
Sosthenes C Amlima
Upendo Mwankenja

**Wanachama wapya**

Tulikuwa na wanachama wapya wanne Amar Shanghavi, Nickson Kilunga, Solomon Mihoyo na Upendo Mwankenja. Walijitambulisha na tulwakaribisha kwenye UWABA.

**Mradi wa Usalama barabarani - Wamba Memorial Fund**

Wanachama tuliongea kuhusu mafunzo ya usalama barabarani tulikuwanayo wiki hii, na kuhusu Andrew Wheeldon kutoka Bicycle Empowerment Network, Afrika Kusini kututembelea. Wanachama tulikubali kwamba mafunzo yaliendelea vizuri sana. Tulikuwa na washiriki 15-17 kutoka UWABA, wawili kutoka HUWATA, watatu waalimu wa shule kutoka Msongole na Kigamboni, mhandisi kutoka TANROADS na mwakilishi kutoka Traffic Police. Wanachama walipenda mada zote tulifundisha na jinsi nzuri tulivyofundishwa. Dominata alipata waandishi wa habari kuhudhuria siku la tatu na habari za mafunzo yalikuwepo kwenye stesheni za radio mbili (Dira, Radio Times na Pata Pata, Wapo Radio) pamoja na gazeti moja (Nipashe).

Kuhusu mipango kwenda mbele, Hussein Hamza na Filbert walipendekeza tufanye mazoezi kufundishana kwanza. Ally Saidi Mohammed alipendekeza tukae kwenye makundi na kila wiki kundi moja wanafundisha mada moja kwa wanachama ambao hakuwepo kwenye mafunzo pamoja na waliokuwepo. Tuliongea kuhusu kupata bao ya nyeusi kwa ajili ya ofisi mpya ambayo itasaidia katika mafunzo (ona dondoo kuhusu ofisi chini). Elaine ataandika repoti ya mafunzo kwa kutumia repoti Andrew aliyoandika na daftari za wanachama. Baada ya kuhamia ofisi na kupata bao ya nyeusi tutachagua kundi.

Edgar alipendekeza kwamba pamoja na kufundisha kozi pia tuende kwenye barabara na uwanja ambapo kuna watu na tunatoa mafunzo pale pia. Pia tulikuwa na wazo kupata waandishi wa habari kuweka mafunzo kwenye TV. Ally Saidi Mohammed alisema tufundishe wazazi pamoja na wanafunzi wa shule.

Juma na Elaine wataandaa reporti ya matumizi ya kifedha ya wiki hii kwa sababu ya matumizi mengi.

**Andrew kutembelea ofisi mbali mbali**

Alhamisi Andrew alitembelea traffic police na TANROADS pamoja na Sosthenes na Juma. Alituandikia reporti na pia Sosthenes alitueleza kuhusu mikutano.

Walikutana na mkurugenzi wa mipango TANROADS ambaye aliunga mkono nasi na alisema UWABA na TANROADS tuendelee kuwasiliana kuhusu mambo ya baisikeli. Andrew alipendekeza tuwe na mkutano wa kila mwezi katika mashirika ya serekali na mashirika ya siyo ya kiserekali kuhusu mambo ya baisikeli, na mkurugenzi alikubali na alisema tuandike wazo hili kwenye barua.

Walichanganye sehemu na muda ya mkutano na traffic police lakini mwishoni walikutana na mtu anayehusika, ambaye alisema tuwaalike traffic police kwenye mikutano yoyote.

Ijumaa walijaribu kutana na Mama Mlamba wa serekali ya jiji lakini walichelewa mkutano na alikuwa na lazima kwenda mkutano mwingine.

Tuliamua kuwaalika TANROADS, serekali ya jiji, traffic police na wengine wanaohusika kwenye mkutano na ajenda iwe kuandaa mikutano ya kila mwezi

Pia tuliongea kwamba tumwulize Engineer Daffa kama TANROADS wanaweza kuwa na safari kupita barabara ya Sam Nujoma kuwaonyesha UWABA, diwani ya halmashauri na wengine njia za baisikeli.

**Ofisi**
Kwa sabara tunatakiwa kuhama kabla ya tarehe 1 mwezi wa nane, tulikubali tuhame jumatatu mchana kuanzia saa sita mchana. Kazi ya kuhamia itafanyika na Aseli Wilson, Filbert Mbecha (ambaye atakuja na guta), Hussein Hamza, Ally Saidi Mohammed (ambaye ataleta vifaa vya kutoa bao za tangazo na rafu) na Juma (ambaye atakuwa na ufunguo wa ofisi mpya).

Ally Saidi Mohammed pia alisema atapata taarifa ya gharama ya vifaa kutengneza bao ya nyeusi, na Amar alisema atatafuta taarifa bei za bao za nyeusi pia. Tulikubali tuwena bao ambazo tunaweza tutembea nazo ili tutumie kwenye mafunzo shuleni pia.

**Msafara wa Baisikeli**
Elaine aliandika upya proposal ya msafara ya baisikeli ya mwaka jana ili kuiandaa ya mwaka huu lakini alisahau kuleta kwenye mkutano – atakuja nayo wiki ijayo.

**Mambo mengine**
Tuliongea kuhusu t-shirt ya BEN ambayo Andrew alitupa na Dominata alikuwa nayo. Sosthenes alipendekeza ibaki ofisini. Baada ya mazumgumzo tulikubali mtu avae ili kutangaza. Tulikubali Dominata awe nayo kwa ajili ya UWABA na avae sana.

Edgar alipendekeza serekali ilazimishe watu kupata mafunzo na alama kutoka UWABA kabla hawajapanda baisikeli lakini wanachama wengine walisema hii itasababisha wapanda baisikeli kukata tamaa na kutopanda baisikeli na itasababisha rushwa.

Dominata alipendekeza wakati tupo ofisini mpya tuzunguke na baiskeli pamoja baada ya mkutano na tuvae t-shirt, helmet na reflective jackets ili tuonekane sana kama chama.

Tulipendekeza tupate watu kufanya documentary ya TV kuhusu UWABA na mambo ya baisikeli Dar es Salaam.

Sosthenes alisema kwamba alisikia Rais Kikwete amesema anahamasisha wapanda baisikeli juzi juzi. Tuliongea kuhusu kumwandikia barua kujitambulisha. Mwisho tuliamua Sosthenes na Dominata wapate taarifa kwanza alisema nini sawa sawa na wapi na lini.

Ally Saidi Mohammed alisema baisikeli ya Kibwana ya walemavu siyo kwenye hali nzuri na sisi wanachama wa UWABA tumsaidie kurekebisha kwa sababu yeye ni mwanachama wa muda mrefu. Tulikubali kwamba wanachama wa UWABA ambao ni wafundi waiangalie na baada ya hapo UWABA na wanachama wa UWABA wachangie kurekebisha.

Bashiri aliomba kwamba wanachama wa UWABA ambao hawakupata helmet kwenye uzinduzi wa ofisi wapate. Elaine alisema kwanza tuandae ili repoti ya fedha ili tuangalie tupo wapi kifedha na tunaweza kuiweka chini ya badjeti gani.